**MWONGOZO KIDATO CHA TATU**

1. **UFAHAMU**

a)

- Lugha za kigeni
- Ushirikiano wa sehemu hizi za Kiafrika na jamii za Kimagharibi. (al. 2✏1=2)

b)

- Kuendeleza lugha zetu ambazo zinatumiwa na wengi
- Kwa kukopa istilahi za kisayansi na kiteknolojia. (al. 2✏1-2)

c)

- Maendeleo mengi yametufikia kupitia kwa lugha za kigeni kama Kingereza, Kifaransa na Kijerumani.
- Harakati madhubuti na mahususi hazijawekwa ili kuifanya lugha hii itumike katika teknohama.
- Panahitajika utafiti madhubuti na juhudi za pamoja kutoka kwa jamii ya kimataifa ili kustawisha Kiswahili. (al. 3✏1=3)

d)

- Matafiti ataweza kupata habari tofauti ambazo zitaweza kufanikisha utafiti wake.
- Mpango wa elimu ya masafa utasaidia kutambua maneno yaliyofanyiwa utafiti kupitia kwa mtandao.
- Wataweza kujua matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanywa katika lugha ya Kiswahili.
- Kujua vipengele vilivyotafitiwa na ambayo havijatafitiwa. (al. 4✏1=4)

e) Ukosefu wa istilahi zinazoweza kutumiwa katika ngazi mbalimbali. (al. 1✏1=1)

f)
- a) Madhubuti – imara
- b) Finyu – iliyobanwa, Isiyopanuka zaidi
- c) Kengeusha – potoshwa katika matumizi ya habari. (al. 3✏1=3)

**2. MUHTASARI**

- Umeme kutokana na maji
- Umeme kutokana na volkeno pamoja na zilizala
- Umeme kutokana na majenereta au vifanyiza vinavyotoa nguvu za umeme.

- Umeme kutokana na jua
- Umeme kutokana na samadi ya wanyama. (al. 4x2=8)

ii)

- Umeme kutokana na maji ndiyo ya kimsingi ya kutolea nguvu za umeme.
- Bwawa hujengwa kwenye mito kuhifadhi maji
- Magurudumu huvingirishwa na nguvu za maji .
- Magurudumu huzungusha nyuzi za shaba zilizowekwa sumaku hivyo kutoa aina moja ya kawi.
- Kawii hii hubadilishwa ili kuvuta nguvu za umeme zilizohitajika
- Umeme unaopatikana husafirishwa kwa kutumia waya hadi vituo mbalimbali. (al. 4x1-=4)

3.**MATUMIZI YA LUGHA**

a) dh -nzito/ ghuna -al.1

th -hafifu/sighuna -al1.

b) i) Juma ni mlevi Ktz al.2

ii) Ameenda darasani -kielezi

c) i) Mtu/watu wamefanya hivyo kwaniaba yao.

ii) Kulazimishwa /kushurutishwa.

d) Nyakati za kiangazi kuna matatizo yanayokumba zaraa. Atakaebadilishia neno kiangazi na zaraa =0

4x ½ =al2.

e) Fatuma alisema kuwa Sofia alikuwa amemletea nguo yake siku iliyotangulia na angeivaa siku ambayo ingefuata akienda Nairobi.

6x ½ =al3.

f) i) Hali ya kuendelea/ kitenzi kishirikishiki kamilifu.

ii) kutowezekana /hamna matumizi

(alama 2)

g) i) Shangazi -kitondo

ii) barua -kipozi alama 3.

iii) posta -Ala.

h)

| | |
|---|---|
| S | KN + KT |
| KN | N + S |
| N | Mganga |
| S | aliyefarikijana |
| KT | T+E |
| T | atazikwa |
| E | kesho. |

8x ½ =al.4

i) Kipaka kilimraruua kinguo chake.

Kijipaka kilimrarua kijinguo chake.

Zozote sahihi =al.2

j) Ungekua nani asiangekusamehe. (al.2)

Akikosa upande mmoja =0.

k) i) Mtu anayekula mkate ameagiza aletewe chai.

ii) Mtu ambaye anakula mkate ameagiza aletewe chai.

iii) Mtu anayemkate ameagiza aletewe chai.Lolote/sahihi =al2.

L) Ni vigumu kwa Watoto wasiothamini wazazi wao kufanikiwa maishani. Al.2

M) Nani aliyekikata chandarua changu kwa wembe? Sasa sitaweza kusafiri nilikotoka kule Malaba. Ninamtaka aje aniombe msamaha.

6x ½ =al3.

N) Kitenzi kishirikishi kipungufu. Wameridhiana.

Kukubali/kusisitiza wa-me-awali- al 1

Kivumishi kiashiria an-a-tamati- al.1

Jinsi/namna. Zozote 2x1=al2.

o) Wanafunzi ambao hupita mtihani husherehekea. al1

p) Mwalimu mwanamke alitufunza. (al. 1) (kadiria)

q) Kirai nomino – walimu wa Kiswahili.

r) Mvulana mmoja ametalikiwa.

Akiandika msichana =0.

Al.1

S) i) Changamanoal.1

ii) Ambatano al.1

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Eleza maana ya lugha ya taifa. (alama 2)

Ni lugha iliyoteuliwa kama kitambulisho cha utamaduni na ustaarabu wa taifa zima.

(1x2=2)

(b) Eleza sababu tatu zinazofanya watu kubadili na kuchanganya ndimi. (alama 3)

i. Kusisitiza ujumbe.

ii. Upungufu wa msamiati wa lugha moja.

iii. Kutaka kudhihirisha uko kundi Fulani la watu. (1x3=3)

(c) Eleza hatua tano ambazo zimesaidia kukuza lugha ya Kiswahili baada ya uhuru nchini Kenya. (alama 5)

i. Kuwekwa kwa sera.

ii. Kueuliwa kwa Kiswahili kama lugha ya taifa.

iii. Vyombo vya habari na mawasiliano mfano taifa leo.

iv. Shughuli za biashara.

v. Uchapishaji wa vitabu.

vi. Shughuli za kidini.

vii. Kampeni za kisiasa vilitegemea matumizi ya Kiswahili. (1x5=5)

Makosa nne ya sarufi adhibu alama mbili

Hijai adhibu alama mbili